JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** HWK/S.1/22/VOL.1/145

02.09.2021

# TANGAZO LA KAZI

**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Korogwe kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la AMREF kupitia mradi wa "Afya kamilifu" anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzani wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi 10 (Kumi) kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.**

1. **Muuguzi Daraja la II,** *nafasi 4 (kituo cha Afya Magoma 1, Kituo cha Afya Mombo 1, zahanati ya Mazinde nafasi 2).*

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- Awe amefuzu mafunzo ya Uuguzi ngazi ya astashahada kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na baraza la Wauguzi Tanzania.
- Awe na uzoefu wa kufanya unasihi na kutoa dawa za ARV kwa watu wanaoishi na VVU.
- Awe anaelewa mfumo unaotumiwa na wizara ya afya na namna unavyofanya kazi, awe anajua namna ya kutumia vitendea kazi mbalimbali vinavyotumika katika kuhudumia watu wanaoishi na VVU.
- Awe na uwezo wa kuongea, kusoma na kuandika Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
- Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja na taarifa zote za wagonjwa.
- Awe uwezo wa kushirikiana na kuchangamana na makundi yote ya watu bila kujali umri au hali walizo nazo pamoja na uwezo wa kuwakaribisha na kuwahudumia watu wote bila unyanyapaa.
- Awe tayari kuishi karibu na eneo lake la kazi.

2. **Tabibu Daraja la II** *nafasi 2 (Kituo cha afya Mombo 1, zahanati ya Mazindo 1)*

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- Awe amefuzu mafunzo ya utabibu ngazi ya stashahada na kusajiliwa na kusajiliwa baraza linalosimamia taaluma husika.
- Awe na uzoefu wa kufanya unasihi, na kutoa huduma za ujumla za kinga, tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU.

Scanned by TapScanner

- Awe na uwezo wa kuongea, kusoma na kuandika Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
- Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja na taarifa za wagonjwa.
- Awe na uwezo wa kushirikiana na kuchangamana na makundi yote ya watu bila kujali umri au hali walizo nazo pamoja na uwezo wa kuwakaribisha na kuwahudumia watu wote bila unyanyapaa.
- Awe tayari kuishi karibu na eneo lake la kazi.

3. **Mteknolojia Msaidizi Maabara** Nafasi 2 *(zahanati ya Hale Sisi kwa Sisi 1,kituo cha afya Mombo 1)*

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- Awe amefuzu mafunzo ya sayansi ya maabara ngazi ya astashahada kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na baraza linalosimamia taaluma husika.
- Awe na uzoefu wa kuchukua na kuzichakata ipasavyo sampuli za HVL kwa wateja wanaoishi na VVU.
- Awe na uwezo wa kuongea, kusoma na kuandika Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
- Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja na taarifa zote za wagonjwa.
- Awe uwezo wa kushirikiana na kuchangamana na makundi yote ya watu bila kujali umri au hali walizo nazo pamoja na uwezo wa kuwakaribisha na kuwahudumia watu wote bila unyanyapaa.
- Awe tayari kuishi karibu na eneo lake la kazi.

4. **Mteknolojia Dawa daraja la II** *nafasi 1(Kituo cha Afya Mombo)*

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- Awe amefuzu mafunzo ya teknolojia ya dawa ngazi ya stashahada kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na kusajiliwa baraza la Famasia.
- Awe na uzoefu wa Uagizaji, Utunzaji na Usambazaji wa Dawa zikiwemo ARVs
- Awe anafahamu vyema mfumo wa moduli ya famasia (Pharmacy Module).
- Awe anaelewa mfumo unaotumiwa na wizara ya afya na namna unavyofanya kazi, awe anajua namna ya kutumia vitendea kazi mbalimbali vinavyotumika katika kuhudumia watu wanaoishi na VVU.
- Awe na uwezo wa kuongea, kusoma na kuandika Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
- Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja na taarifa zote za wagonjwa.
- Uwezo wa kushirikiana na kuchangamana na makundi yote ya watu bila kujali umri au hali walizo nazo pamoja na uwezo wa kuwakaribisha na kuwahudumia watu wote bila unyanyapaa.
- Awe tayari kuishi karibu na eneo lake la kazi.

*Scanned by TapScanner*

5. **Karani Wa Takwimu (Data Clerk)** *nafasi 1(zahanati ya Mazinde)*

- Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- Awe na uelewa mzuri katika matumizi ya kompyuta.
- Awe na uzoefu wa Uingizaji naUtunzaji taarifa za mfumo wa uendeshaji huduma za Afya.
- Awe anafahamu vyema mfumo wa Electronic CTC-2 data base na kuweza kutengeneza na taarifa mbalimbali kutoka katika mfumo huo.
- Awe na uwezo wa kuongea, kusoma na kuandika Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
- Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja na taarifa zote za wagonjwa.
- Awe na uwezo wa kushirikiana na kuchangamana na makundi yote ya watu bila kujali umri au hali walizo nazo pamoja na uwezo wa kuwakaribisha na kuwahudumia watu wote bila unyanyapaa.
- Awe tayari kuishi karibu na eneo lake la kazi.

**Mishahara**

Mishahara italipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali

Waombaji wanahimizwa kuambatisha nyaraka zifuatazo:-
(i) Barua ya maombi ya kazi
(ii) Nakala ya cheti cha kidato cha nne/sita;
(iii) Nakala ya vyeti vya taaluma;
(iv) Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
(vi) Maelezo binafsi (CV), yakionesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani pamoja na anuani/namba za simu za kiganjani za wadhamini wasiopungua wawili.

*Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani hii:-*

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya Korogwe,**
**S.L.P. 584,**
**Korogwe.**

**Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 18 Septemba 2021**

Halfan H. Magani
**Mkurugenzi Mtendaji(W)**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 584
KOROGWE



*Scanned by TapScanner*